**TAARIFA FUPI YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA UWASILISHAJI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI MKOANI RUKWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2023 HADI JUNI, 2024.**

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana Mahali hapa tukiwa wazima na wenye Afya njema. Aidha nikushukuru sana wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wetu wa Rukwa pamoja na Kamati yako ya Siasa ya Mkoa kwa maoni na Mapendekezo mbalimbali mnayonipatia wakati wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 - 2025 Mkoani kwetu Rukwa. Kipekee nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupatia fedha nyingi za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika Mkoa wetu. Hakika tangu ameingia Madarakani mwaka 2021 amekuwa ni kielelezo cha Maendeleo ya Wanarukwa na Watanzania kwa ujumla.

***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe,*** Tarehe 15 -18 Julai, 2024 Mkoa wetu ulipokea uongozi mkubwa wa Kitaifa wa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambae alifanya ziara Mkoani Rukwa na kuweka mawe ya Msingi, kuzindua Miradi na kuzungumza na Wananchi. Nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi, Viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi, Wananchi na Makundi mbalimbali ya Wananchi kwa ushirikiano mliotupatia mpaka kufanikisha ziara hiyo ambayo ilifana sana Mkoani kwetu. **Asanteni sana.**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Katika kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuwaletea Wananchi Maendeleo; Mkoa umeendelea na juhudi za kutoa huduma bora za kiuchumi na kijamii kwa Wananchi kwa kuboresha huduma za Afya, Elimu, Barabara, Upatikanaji umeme, Maji na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wananchi. Sambamba na hilo Viongozi wa ngazi zote katika Mkoa walielekezwa kwenda kwa Wananchi kutatua kero mbalimbali na kwa wakati.

***Ndugu Mwenyekiti,*** Hali ya Usalama Mkoani Rukwa ni shwari, Matukio mbalimbali yanayojitokeza yamekuwa yakidhibitiwa na vyombo vyetu vya Usalama. Sambamba na hilo katika kudhibiti Matukio ya Ujambazi katika Ziwa Tanganyika hasa utekaji kwa Wavuvi tumeendelea kuimarisha Ulinzi mwambao mwa ziwa Tanganyika kwa kutumia Viteule vyetu vya Jeshi la Wananchi vya Kirando, Kipili na Kasanga na Polisi Wana Maji Kipili. Aidha tumefanikiwa kujenga kituo cha Polisi cha Kisasa katika Kijiji cha Mpasa Kata ya Kala.

***Ndugu Mwenyekiti,*** Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais na Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi Taifa imepata Mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 kama ifuatavyo:-

**i. Ukusanyaji wa Mapato**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Kwa upande wa ukusanyaji wa Mapato Jumla ya shilingi 17,867,761,011.81 zilikusanywa na TRA kwa kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni,2024 ambapo TRA ilivuka lengo la kukusanya shilingi Bilioni 17,752,344,478.48 kwa kipindi hicho sawa na Asilimia 101.

Kwa upande wa Mapato ya Halmashauri Jumla ya shilingi Bilioni 10,904,156,336.12 zilikusanywa na Halmashauri zote nne za Mkoa wa Rukwa sawa na asilimia 93 ya kukusanya shilingi Bilioni 11,700,527,400.00

**ii. Miradi ya Sekta ya Utawala Bora**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Juni, 2024 Jumla ya shilingi Bilioni 2, 836, 794,393.24 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Ofisi na nyumba za makazi ya viongozi Kazi zilizofanyika ni Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi,Ujenzi wa nyumba mpya ya Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Ujenzi wa Ofisi 2 za Tarafa ya Matai na Kate, na Ukarabati wa nyumba za Viongozi na Wakuu wa Seksheni,Ukarabati wa Ukumbi wa Mikutano na Utengenezaji wa samani za Ofisi.

**iii. Sekta ya Afya**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Ibara ya 83 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatoa msisitizo kwa chama cha Mapinduzi kuendelea kutoa kipaumbele kwa Afya za Wananchi.Katika Kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilitoa jumla ya shilingi Bilioni 2,320,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo ya Sekta ya Afya.Fedha hizo zimetumika kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga ya Isofu na, Kujenga Vituo vya Afya Viwili na umaliziaji wa Zahanati 15. Miradi hii inaendelea vizuri na ile ambayo bado haijakamilika naahidi kuwa tutaikamilisha kwa wakati ili Wananchi wapate huduma.

**iv. Miradi ya Elimu**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Ibara ya 80 ya ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 inasisitiza umuhimu wa Chama cha

Mapinduzi kutambua umuhimu wa Elimu. Katika kutekeleza hilo serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 imeidhinisha jumla ya shilingi Bilioni 8,239,190,627.75 ambazo zimetumika kujenga Madarasa ya Msingi 84, Matundu ya vyoo 388, Shule Mpya za Msingi (3), Mabweni 2 shule za Msingi Maalum na Uzio 1 shule ya Msingi Maalum kule Muze. Kwa upande wa Sekondari zimejenga Matundu ya vyoo 245, Madarasa 170, na Shule Mpya za Sekondari saba 7, Mabweni kumi na mbili (12) yamejengwa, Maabara (4) zimejengwa na Ujenzi wa nyumba za Walimu tano (5). Kujengwa kwa Miundombinu katika shule za Msingi na Sekondari kumesaidia sana kupunguza msongamano wa Wanafunzi Madarasani na kupunguza umbali wa Wanafunzi kufuata huduma ya Elimu. Pamoja na ujenzi wa miundombinu hiyo ya Shule za Msingi na Sekondari; Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Tawi la Rukwa kilichopo eneo la Kianda pia kimeidhinishiwa jumla ya shilingi Bilioni 14,679,637,853.57 kwa ajili ya jengo la taaluma (Academic Block), Majengo ya kalakana na barabara za kuzunguka Chuo hicho ambapo ujenzi bado unaendelea. Aidha kujengwa kwa Chuo kikuu kishiriki cha Sayansi na Teknolojia Tawi la Rukwa kitasaidia Mkoa katika kuleta Teknolojia Mpya ya Kilimo na Ujenzi. Aidha kitasaidia kukua kwa Kijiji cha Kianda na hatimaye uchumi wa Wananchi waishio katika eneo hilo utakua kwa kufanya biashara mbalimbali. Sambamba na hilo Watoto wetu wa Mkoa wa Rukwa watapata nafasi ya kupata Elimu ya Chuo Kikuu.

**V. Miundombinu ya Barabara (Tanroads).**

**(a) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Sumbawanga.**

***Ndugu Mwenyekiti*** Ujenzi wa Uwanja wa ndege Sumbawanga unaendelea vizuri chini ya Mkandarasi MS SINO SHINE EAST AFRICA LTD. Mpaka kufikia mwezi Juni, 2024 Mradi ulikuwa umefikia asilimia

15.82 ya utekelezaji.Gharama ya Mradi wa ujenzi na ukarabati wa uwanja wa ndege wa Sumbawanga ni shilingi Bilioni 60.

**(b) Barabara za Tanroads.**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Kwa upande wa Barabara za TANROADs Mkoa unaendelea na ujenzi wa Barabara ya Ntendo -Muze-Kilyamatundu Sehemu ya Ntendo -Kizungu Kilometa 25 kwa gharama ya shilingi Bilioni 45,299,852,298.00. Changamoto za malipo ya Wakandarasi kama Mkoa tutaendelea kufuatilia ili malipo yafanyike kwa wakati na miradi hiyo kukamilika kwa wakati. Aidha ujenzi wa Barabara ya Matai- Kasesya KM 50 tumeanza kujenga KM 25 za Matai -Tatanda kwa gharama ya shilingi Bilioni 37,353,089,366.00. Aidha ujenzi wa KM 25 zingine za Tatanda - Kasesya tayari tumeanza taratibu za kulipa fidia ili tuanze kujenga kipande hicho kilicho salia.

**(c) Barabara za Mjini na Vijijini**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Ibara ya 57 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inasisitiza uboreshaji wa Miundombinu ya Mjini na Vijijini. Katika kutekeleza hilo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 TARURA wamesaini jumla ya mikataba 36 yenye thamani ya shilingi Bilioni 8, 538,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara za Mjini na Vijijini. Kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa na Rais wetu kwa kuiongezea TARURA Bajeti kutoka Bilioni 5 mwaka 2021 hadi Bilioni 8 mwaka 2023/2024 ambayo kwa kiasi kikubwa imeboresha Barabara zetu za Mjini na Vijijini licha ya Changamoto za Mvua ambazo zimeikumba nchi yetu na kuharibu miundombinu ya Barabara.

***Ndugu Mwenyekiti,*** Kupitia Mradi wa kuboresha Miji (TACTIC) tumepokea shilingi Bilioni 20,361,688,071 kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha Lami KM13 Manispaa ya Sumbawanga pamoja na eneo la kuzunguka Hospitali ya Isofu. Barabara hizi zikikamilika zitasaidia Wananchi wetu kupita, kuimarisha biashara katika maeneo hayo pamoja na kupendezesha Mji.

**vi.Sekta ya Maji**

***Ndugu Mwenyekiti,*** Ibara ya 100 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inasisitiza umuhimu wa kuboresha upatikanaji wa maji na kufikia asilimia 85 ya upatikanaji wa Maji Vijijini na Asilimia 95 Mijini. Katika Kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 jumla ya Shilingi Bilioni 16,690,071,684.22 zimepokelewa kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya Maji 33 yenye thamani ya shilingi Bilioni 88,012,454,097.15 Asilimia ya Upatikanaji wa Maji Vijijini imeongezeka na kufikia Asilimia 61 na Mjini asilimia ya upatikanaji wa Maji imeongezeka na kufikia Asilimia 95.

**Ndugu Mwenyekiti,** Maelekezo yako ya Kikao cha Kamati ya Siasa Mkoa niliyachukua na nitayafanyia kazi mimi pamoja na wenzangu. Barabara ya Chombe –Kiandaigonda –Kaoze nimewaelekeza TARURA kuhakikisha kuwa wanapeleka Ombi maalumu Wizarani ili tuweze kupata fedha za kukamilisha Barabara hiyo, Aidha nimemuelekeza Katibu Tawala wa Mkoa kuhakikisha kuwa anamsimamia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ili akamilishe Zahanati ya Kijiji cha Mlenje kata ya Legeza mwendo ili wananchi wale waliopo mpakani waweze kupata huduma. Sambamba na hilo nimewaelekeza Wakuu wa Wilaya wote pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa kwa kushirikiana na Wananchi wanatatua changamoto ya Madawati.

**Ndugu Mwenyekiti,** Uharibifu wa mazingira katika Mkoa wetu umekuwa ukiongezeka. Kupitia kikao chako niwaagize Wakuu wangu wa Wilaya na

Wakurugenzi wote kuhakikisha kuwa Wanazingatia na kuitekeleza sheria ya mita 60. Sambamba na hilo Milima ya Lyamba lya Mfipa itunzwe ili kuepuka uharibifu wa Mazingira.
Ndugu Mwenyekiti, Ununuzi wa Mahindi kupitia Wakala wa uhifadhi wa Chakula (NFRA) unaendelea vizuri ambapo Mpaka sasa Jumla ya Tani 18,797.044 zimekwisha nunuliwa na NFRA. Tunamshukuru sana Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuwaongezea bei Wananchi wetu wa Mkoa wa Rukwa ambao kwa asilimia kubwa ni Wakulima.

***Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe**,* Taarifa yangu hii ni Mhutasari tu wa taarifa kubwa ya Utekelezaji wa Ilani ambayo inaonesha Miradi iliyotekelezwa kwa kirefu kuanzia Sekretarieti ya Mkoa, Taasisi za Mkoa na Halmashauri.

***Ndugu Mwenyekiti,*** Mwisho lakini si kwa umuhimu nitumie fursa hii adhimu kukushukuru sana wewe mwenyewe kwa usimamizi wako Madhubuti wa Serikali yako ya Mkoa pamoja na Wenyeviti wa Wilaya kwa namna wanavyosimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwenye Wilaya zao. Aidha nikuhakikishie tu kuwa Miradi yote ya Maendeleo itakamilika kwani tulipotoka sio sawa na hapa tulipo na tuendako ni neema. Wakati wa kusoma utekelezaji wa Ilani Mwaka Jana hali ya utekelezaji wa Miradi kwenye Mkoa wetu ilikuwa ni ya kusuasua lakini chini ya uongozi wako Mwenyekiti wetu wa CCM wa Mkoa Miradi mingi sasa inakamilika na kuanza kutumika. Niseme tu kwa utekelezaji huu wa Miradi ya Maendeleo kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka huu 2024 ni ishara kuwa tutapata ushindi wa kishindo. Aidha kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwakani tutapata ushindi wa kishindo wa Mhe. Rais, Wabunge na Madiwani.

**Mwisho** lakini si kwa umuhimu nimshukuru sana Katibu Tawala wangu wa Mkoa wa Rukwa kwa weredi wake mkubwa wa kuwasimamia Watendaji ndani ya Mkoa, Aidha niwashukuru sana Wakuu wangu wa Wilaya kwa kunisaidia vyema kusimamia utekelezaji wa Ilani. Wapo pia Wakuu wa Sehemu na Vitengo, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi za umma ndani ya Mkoa, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata na Vijiji na Watumishi wote wa umma ndani ya Mkoa wetu wa Rukwa, Sambam,ban a hao wapo Wahe. Wabunge nawashukuru sana kwa ushirikiano wao, Mstahiki Meya, Madiwani na Wenyeviti wa Halmashauri nawashukuru sana kwa ushirikiano wakati wote wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Hawa wamekuwa chachu ya Maendeleo tunayoyapiga ndani ya Mkoa wetu wa Rukwa.

Mhe. Mwenyekiti, Niwashukuru sana Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa ngazi zote. Wamekuwa ni faraja sana kwangu wakati wa utekelezaji wa Majukumu yangu. Kila nikienda kwenye Ziara nawakuta kule na huwa nafarijika sana. Hakika Mhe. Mwenyekiti una majembe kweli kweli.

**Mungu Ibariki Tanzania,**
**Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,**
**Mungu Kibariki Chama chetu cha Mapinduzi**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**